
JIMBO KUU LA DAR ES SALAAM

PAROKIA YA MT. POLYCARP ASKOFU NA SHAHIDI – KILAMBA



Padre Alphonce Ntakwizile

PAROKO

Viongozi Kamati Tendaji Halmashauri Walei Parokia 2023 - 2025



Herman Lyoba

Mwenyekiti H/W.



Samweli Ndomba

M/Mwenyekti H/W.



Godeliva Mutakyawa,

Katibu H/W.



Godfrey Mwangailo,

Katibu Msaidizi H/W



Monica Mwogofi

Mweka Hazina H/W

UONGOZI WA PAROKIA YA MT. POLYCARP ASKOFU NA SHAHIDI – KILAMBA AMBAO PIA NI WAANZIRISHI WA PAROKIA.

HISTORIA YA PAROKIA

Utangulizi

Parokia ya Mt. Polycarp Askofu na Shahidi Kilamba, ni moja kati ya parokia za jimbo kuu la Dar Es salaam. Parokia hii ilianza tarehe 06/07/2019 ikiwa ya 117, baada ya kupandishwa hadhi kutoka parokia Teule. Kabla ya hapo Parokia hii ilikuwa kigango cha Parokia ya Mt. Martin wa Tours Kizinga, ambacho kilipandishwa hadhi kuwa Parokia teule tarehe 07/07/2018. Kigango cha Mt. Polycarp Askofu na Shahidi Kilamba kilianza 26/07/2014 baada ya iliyokuwa mitaa ya Parokia ya Mt. Anthony wa Padua Mbagala Zakhemu kuhamishiwa parokia ya Kizinga. Parokia inakadiriwa kuwa na waamini wapatao 3,300 wanaotokana na kaya 828. Kaya hizi zinazounda Jumuiya 35 na Kanda 18.

Mahali Parokia ilipo

Parokia ya Mt. Polycarp Askofu na Shahidi Kilamba, iko katika eneo la kiserikali la Mitaa ya Nzasa A na Nzasa B iliyoko kata za Kilungule na Charambe, wilaya ya Temeke mkoa wa Dar es salaam. Parokia hii inapakana na Parokia ya Mt. Anthony wa Padua Zakhemu upande wa mashariki na kusini, Mt. Clara wa Asizi Chamazi upande magharibi, Kutukuka kwa msalaba Kizuiani upande wa kaskazini na Martin wa Tours Kizinga upande wa kaskazini magharibi.

Maendeleo ya Parokia

Kiwanja cha kanisa ambapo pamejengwa kanisa, nyumba ya mapadri na miundombinu mingine ya kanisa kiligawiwa kwa kanisa mwaka 1994 Kulingana na ramani ya kiwanja (survey plan), kiwanja hiki kinaukubwa wa mita za mraba 7,445. Baada ya kanisa kugawiwa eneo hili utaratibu wa umiliki kisheria ulifanyika na kufuatiwa na uendelezaji unaoendelea mpaka sasa (2019) kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu zilizopo. Uendelezaji wa eneo hili mwanzoni ulisuasua kutoka na migogoro iliyokuwa inaibuka toka jamii ambao sio wakristo, waliokuwa wakipinga eneo hili kupewa kanisa. Migogoro hiyo imekuwa ikitatuliwa pindi inapoibuka, na mpaka sasa hali ni salama na uendelezaji wa eneo unaendelea kama ulivyopangwa.

Waamini kutoka jumuiya na mitaa/kanda wanaozunguka eneo hili wamekuwa wakifanyia mikutano yao ya jumuiya toka eneo kugawiwa kanisa mpaka sasa, na wao ndio wamekuwa walinzi na wasimamiaji wa eneo hili. Aidha toka kupewa eneo hili misa takatifu za kijumuiya na kikanda/kimtaa zilikuwa zinafanyika kwa kutumia mahema. Kutokana na maelekezo ya kanisa parokia hii ilianza ikiwa kituo cha sala, baadaye kigango, ikafuata parokia teule na mwisho Parokia. Hii ilitokana na waamini kuongezeka katika eneo, umoja na mshikamano wa waamini, majitoleo yao kwa kanisa na ushiriki wao katika ibada na matukio mbalimbali ya kanisa ndani na nje ya Parokia. Haya yote yalitosha kushawishi uongozi wa kanisa kijimbo kutangaza kuwa Parokia.

Uongozi

Viongozi waanzilishi wa parokia hii ni kama ifuatavyo.

1. Padre Alphonce Ntakwizile Paroko-simu namba: 0759 129 442
2. Herman Lyoba Mwenyekiti H/Walei Parokia – simu namba: 0755 576 412
3. Samweli Ndomba Makamu mwenyekiti H/Walei Parokia – simu namba:0784 670 524
4. Godeliva Mutakyawa Katibu H/Walei Parokia – simu namba: 0784 708 726
5. Godfrey Mwangailo Katibu Msaidizi H/Walei Parokia – simu namba: 0788 760 925
6. Monica Mwogofi Mhazini H/Walei Parokia – simu namba: 0782 592 048

Vyama vya Kitume

Parokia imeanzishwa ikiwa na vyama vya kitume kama ifuatavyo

1. Utume wa wanaume katoliki (UWAKA)
2. Utume wa wanawake katoliki (WAWATA)
3. Utume wa vijana wafanya kazi (VIWAWA)
4. Utume wa utoto Mtakatifu
5. Moyo Mtakatifu wa Yesu
6. Karismatiki
7. Shirikisho la kwaya la Parokia (SHIKWAKI)
8. Watumishi wa altare

Litrujia

Parokia ina kwaya 3 ambazo ni Kwaya ya Mt. Polycarp Askofu Shahidi, Kwaya ya Mt. Donbosco na kwaya ya Mt. Theresia wa Mtoto Yesu, ambayo ni ya utoto mtakatifu. Siku za dominica Parokia ina Misa 3. Na siku za wiki ina misa kila asubuhi saa 12.30 ikitanguliwa na Masifu isipokuwa Alhamisi. Alhamisi ni siku ya kuabudu Ekaristi Takatifu kuanzia saa 11.00 Jioni ikifuatiwa na Misa takatifu.

Mawasiliano

Barua pepe: **mtpolycarp@gmail.com**; Sanduku la Posta: **167, Dar Es Salaam** Simu zinazotumika ni za Paroko na Halmashauri walei